



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**TAARIFA KWA UMMA**

**KUHUSU RATIBA YA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE**  
**KATIKA JIMBO LA ARUMERU MASHARIKI**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepokea barua kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye kwa kuzingatia kifungu cha 37(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 ya Sheria za Tanzania aliitaarifu Tume kuwepo kwa nafasi wazi ya Ubunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru mkoani Arusha.

Kwa mujibu wa barua hiyo ya Spika, nafasi hiyo wazi imetokana na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo Ndg Joshua Samwel Nassari kupoteza sifa ya kuwa Mbunge baada ya kutohudhuria mikutano ya Bunge mitatu mfululizo bila ruhusa ya Spika.

Kwa kuzingatia masharti ya vifungu vya 37(1)(b), na 46 (2) vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Tume inautaarifu Umma kuhusu ratiba ya uchaguzi mdogo katika Jimbo hilo kama ifuatayo:

1. Fomu za Uteuzi wa Wagombea zitatolewa kati ya tarehe 15 - 19 Aprili, mwaka huu.
2. Uteuzi wa Wagombea utafanyika tarehe 19 Aprili, mwaka huu
3. Kampeni za Uchaguzi zitafanyika kati ya tarehe 20 Aprili, 2019 hadi tarehe 18 Mei mwaka huu.
4. Siku ya Uchaguzi itakuwa ni tarehe 19 Mei mwaka huu.

Tunapenda kuvikumbusha Vyama vya Siasa na wadau wote wa Uchaguzi kuzingatia Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi, Taratibu, Miongozo na maelekezo yatakayotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakati wa kipindi chote cha Uchaguzi huu mdogo.

Imetolewa leo tarehe 31 Machi mwaka huu.

Jaji (Rufaa) Semistocles S. Kaijage

**MWENYEKITI**

**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**